

# **MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI ZANZIBAR (ZURA)**

## **TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

Mamlaka ya Udhubiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA), imeanzishwa chini ya Sheria Namba 7 ya 2013 ikiwa na jukumu la kusimamia huduma za Maji na Nishati hapa Zanzibar.

ZURA kwa uwezo na mamlaka iliyonayo chini ya Kifungu Nambari 16 (c) ya Sheria Namba 7 ya 2013 inawatangazia wananchi wenye sifa, kuomba nafasi za ajira kama zifuatazo katika Afisi zake za Unguja na Pemba.

### **1. Afisa Manunuzi na Ugavi Mkuu Daraja la Kwanza – Nafasi 1 Unguja.**

#### **Sifa za Muombaji:**

- Awe na Shahada ya Kwanza au Shahada ya Uzamili ya Manunuzi na Ugavi au fani inayolingana na hiyo kutoka katika chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
- Awe na uzoefu wa kazi usiopungua miaka mitano (5), miaka mitatu (3) kati ya hiyo awe ametumikia katika nafasi anayoiomba.
- Awe na ujuzi wa kutumia kompyuta.

### **2. Mkaguzi Nishati Mafuta Daraja la Pili – Nafasi Mbili, 1 Unguja na 1 Pemba.**

#### **Sifa za Muombaji:**

- Kuajiriwa mwenye Shahada ya kwanza katika fani za Nishati ya Mafuta, gesi au inayolingana na hizo kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
- Awe na ujuzi wa kutumia kompyuta.

### **3. Mchumi/Mchambuzi Fedha Daraja la Pili – Nafasi 1 Unguja.**

#### **Sifa za Muombaji:**

- Awe na Shahada ya Kwanza ya Uchambuzi wa fedha (Financial Analysis) Uchumi (*Economics*), Mipango ya Uchumi (*Economic*

*Planning*) au fani inayolingana na hizo kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

- Awe na ujuzi mkubwa katika matumizi ya kompyuta.

#### **4. Afisa Mtatuzi wa Migogoro Daraja la Pili. Nafasi 1 Pemba.**

##### **Sifa za Muombaji:**

- Awe na Shahada ya Kwanza ya Utatuzi wa Migogoro, Sheria, Ustawi wa Jamii au fani inayolingana na hizo kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
- Awe na ujuzi wa kutumia kompyuta.
- Awe amefanya mafunzo ya vitendo ya Sheria (Legal Internship)

#### **5. Afisa Utawala Daraja la Pili – Nafasi 1 Unguja.**

##### **Sifa za Muombaji:**

- Awe na Shahada ya Kwanza ya Utawala wa Umma, Rasilimali Watu au fani inayolingana na hizo kutoka katika chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
- Awe na ujuzi wa kutumia kompyuta na utunzaji wa kumbukumbu.

#### **6. Afisa Usalama na Mazingira Daraja la Pili. Nafasi 1 Unguja.**

##### **Sifa za Muombaji:**

- Awe na Shahada ya Kwanza katika fani ya Sayansi ya Mazingira/Afya na Usalama au fani inayolingana na hizo kutoka katika chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
- Awe na ujuzi wa kutumia kompyuta.

### **TAARIFA ZA JUMLA**

- Muombaji atakaechaguliwa kufanya usaili, usaili huo utafanyika katika katika ukumbi ambao Mamlaka itaamua na kuwataarifu waombaji.
- Muombaji atakaefanikiwa kuajiriwa anatakiwa awe tayari kufanya kazi katika Afisi yoyote ya ZURA ya Unguja na Pemba.
- Muombaji anatakiwa asiwe muajiriwa wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
- Awe tayari kufanya kazi yoyote atakayopangiwa na Mamlaka.
- Muombaji anatakiwa awe Mzanzibari.

## **TAREHE YA MWISHO WA MAOMBI**

Maombi yataanza kupokelewa kuanzia leo tarehe 10/04/2018 na mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 14/04/2018.

## **NAMNA YA KUWASILISHA MAOMBI**

Waombaji wote wanatakiwa kuwasilisha barua za maombi zilizoandikwa kwa mkono, katika Afisi za Kuu ya ZURA na kuambatanisha na vivuli vya taarifa zifuatazo:

- 1) Vyeti vya kumalizia masomo
- 2) Maelezo Binafsi (CV)
- 3) Cheti cha kuzaliwa
- 4) Picha mbili za paspoti zilizopigwa karibuni
- 5) Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi

Maombi yote yawasilishwe katika anuani ifuatayo:

**MKURUGENZI MKUU,  
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI (ZURA),  
S.L.P 2238, GHOROFA YA PILI, JENGO LA MFUKO WA BARABARA,  
MAISARA,  
ZANZIBAR.**

## **ANGALIZO**

KWA MAELEZO ZAIDI KUHUSIANA NA TANGAZO HILI, FUATILIA KATIKA TOVUTI YA ZURA [www.zura.go.tz](http://www.zura.go.tz) AU TUME YA UTUMISHI SERIKALINI NA GAZETI LA ZANZIBAR LEO.